

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

Simu: +255 026 23222761-5
Fax No. +255 026 2322624
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
Mtaa wa Makole
S.L.P. 941,
DODOMA.

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU KUANZA KWA
VIKAO VYA KAMATI ZA BUNGE TAREHE 18 JANUARI HADI
31 JANUARI, 2021 JIJINI DODOMA.**

Kamati za Kudumu za Bunge zitaanza kukutana siku ya Jumatatu tarehe 18 hadi 31 Januari, 2021 Jijini Dodoma kutekeleza majukumu ya kibunge kabla ya Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Mbili uliopangwa kuanza tarehe 02 Februari, 2021.

Kwa mujibu wa ratiba ya shughuli za Kamati, Waheshimiwa Wabunge wote wanatakiwa kuwasili Jijini Dodoma Jumapili tarehe 17 Januari, 2021 tayari kwa ajili ya kuanza kwa vikao vya Kamati. Shughuli za Kamati za Bunge katika kipindi hicho ni kama ifuatavyo:-

A. UCHAGUZI

Kamati zote za Kudumu za Bunge zitafanya uchaguzi wa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti.

B. MAFUNZO

Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge watapewa mafunzo kwa utaratibu ufuatao:-

- (i) Mafunzo kuhusu Majukumu na Taratibu za Uendeshaji wa kila Kamati.
- (ii) Mafunzo kuhusu Bunge Mtandao na Usalama wa Mtandao kwa Kamati zote.

- (iii) Kamati za Kisekta zitapokea maelezo ya Wizara kuhusu Muundo, Majukumu ya Taasisi pamoja na Sera na Sheria zinazosimamiwa na Wizara hizo.
- (iv) Mafunzo kwa Kamati za Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC) na Kamati ya Bajeti kuhusu uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Msajili wa Hazina (TR) na namna bora ya kuhoji Maafisa Masuuli.
- (v) Mafunzo kwa Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo na Uzoefu wa Mabunge mengine ya nchi zinazofuata mfumo wa Kibunge wa Jumuiya ya Madola.

C. **SHUGHULI ZA KAMATI YA BAJETI**

Kamati ya Bajeti itapokea na kujadili:-

- (i) Taarifa ya tathimini ya utekelezaji wa Mpango wa pili wa Maendeleo ya Taifa kwa miaka mitano, 2016/17-2020/21;
- (ii) Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano, 2021/22-2025/26;
- (iii) Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka mmoja 2021/22;
- (iv) Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022;
- (v) Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali pamoja na Sheria ya Fedha kwa kipindi cha nusu mwaka, kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.

Ratiba ya Shughuli za Kamati za Bunge inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni www.parliament.go.tz

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
DODOMA.

13 Januari, 2021.